

# HUDUMA YA UPIMAJI NA RAMANI

## 1.0 Majukumu ya Idara

Upimaji na Ramani ni Idara katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Jukumu lake kubwa ni usimamizi wa upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani mbalimbali za nchi mijini na vijiji. Ramani hizo ni msingi wa kubuni, kupaanga, kutekeleza na kuratibu mipango ya maendelezo juu ya ardhi katika sekta na kwa matumizi mbalimbali kama:

- Umilikishaji ardhi
- Kupanga matumizi ya ardhi
- Utalii
- Mawasiliano
- Makazi
- Kilimo
- Hifadhi ya mazingira
- Utafiti na uchimbaji madini
- Mgawanyo wa Huduma za kijamii nchini.



Urasimu ramani

## 2. Ramani

### 2.1 Ramani zinazotayarishwa

Ramani za msingi kutokana na picha za anga (base maps):

- Ramani za topographia za skeli ya 1:50,000 kwa nchi nzima
- Ramani za maeneo ya mijini katika skeli ya 1:2,500 au 1:5,000
- Ramani za kuzalisha kutokana na ramani za msingi
- Ramani katika skeli ya 1:250,000
- Ramani za mikoa na Wilaya katika skeli ya 1:300,000-1:500,000
- Ramani za masomo maalum
- Ramani ya barabara ya Tanzania katika skeli 1:2.5 m
- Ramani ya jiji la Dar es Salaam katika skeli ya 1:20,000
- Ramani ya utalii ya mlima Kilimanjaro katika skeli ya 1:1 00,000

### 2.2 Picha za Anga

Idara ya Upimaji na Ramani ina maktaba ya picha za anga za sehemu mbalimbali za nchi zilizopigwa katika nyakati mbalimbali tangu miaka ya 1940.

- Picha za skeli ndogo chini ya 1:50,000
- Picha za skeli ya kati 1:20,000-1:50,000
- Picha za skeli kubwa zaidi ya 1:20,000

## 2.3 Uchoraji na Uchapaji wa Ramani

- Tafsiri na utambuzi wa alama katika picha kwa madhumuni ya kuchora ramani, matumizi ya adhi na uoto juu yake.
- Uchoraji ramani kwa mitambo ya photogrammetry
- Usanifu wa ramani
- Utoaji nakala za ramani au plani katika filamu kwa Kamera maalum
- Ukuzaji wa nyaraka kwa njia ya Kamera hadi x 6
- Kushona vitabu

## 2.4 Bidhaa Maalum

Idara ina uwezo kivifaa na kitaaluma kutayarisha ramani, na kutoa huduma mbalimbali kukidhi mahitaji ya wateja kama zifuatazo:

- Ramani maalum kulingana na ubunifu wa vigezo vyta mteja
- Picha-ramani(orthophoto)
- Muunganisho wa picha nyingi kuwa moja-Photo mosaic.
- Ramani katika mfumo wa electronic-digital maps.
- Ramani ya awali iliyochorwa kwa mashine za photogrammetry
- Kumbukumbu Kuu ya uoto kwa nchi nzima (katika mfumo wa electronic)
- Picha za anga katika mfumo wa electronic.

### **3. UPIMAJI TOPOGRAFIA**

#### **3.1 UPIMAJI**

Idara ina uwezo kivifaa na kitaaluma kufanya upimaji wa aina mbalimbali

- Upimaji miliki ukubwa wowote mahali popote nchini
- Upimaji wa kuweka mifumo ya alama za msingi za upimaji
- Upimaji kwa ajili ya utayarishaji wa ramani kutokana na picha za anga
- Upimaji kwa kazi za uhandisi kama vile miinuko, ubapa wa barabara na mapito ya njia za mawasiliano.
  
- Kuchapa ramani katika rangi nyingi au moja hadi ukubwa wa 30" x 40"

#### **3.2 Uwezo wa kupima na kuchora ramani kwa teknolojia ya Kompyuta**

- Uchoraji wa ramani kwa kutumia mashine zilizoshikizwa na Kompyuta
- Upimaji ardhi kwa kutumia kifaa cha *total station* ambacho hunasa vipimo na takwimu moja kwa moja katika mfumo wa electronic.
- Upimaji kwa vifaa vya GPS ambavyo hutumia mawasiliano ya Satellites.
- Kupata ramani ya mwinuko na mabonde usawa wa bahari.
- Usanifu wa ramani kwa kompyuta
- Kuchapa ramani kutoka kwenye kompyuta katika rangi moja au ny ingi.


#### **.Teknolojia ya kisasa**

Kwa kutumia teknolojia ya kisasa, Idara ina uwezo wa kuchora na kutoa ramani katika mfumo wa electronic. Ramani za baadhi ya maeneo hususan ya kati ya jiji na Manispaa zote nchini ziko katika mfumo wa electronic. Ramani au kumbukumbu Kuu ya uoto wa Tanzania ipo katika mfumo wa electronic.

#### **45.Upatikanaji wa bidhaa na huduma za Idara**

**5.1** Bidhaa za kawaida zikiwemo ramani, picha za anga huuzwa katika duka la ramani lililopo jengo la Casino katika makutano ya Barabara ya Kivukoni Front na Luthuli, jijini Dar es Salaam.

#### **Bidhaa na huduma muhimu hupatikana kwa maombi ya mteja**



### **UPIMAJI MILIKI UTANGULIZI**

Lengo la upimaji wa ardhi ni kupata kielelezo halisi na cha kipekee cha utambulisho wa kipande cha ardhi hususan sehemu kilipo, umbile na ukubwa wake na uhusiano wa mazingira yanayokizunguka.

Ili mwanachi aweze kupata hati yake ya kumiliki ardhi, hakuna budi kuwa na kumbukumbu ya mipaka ya kipande cha ardhi husika. Upimaji wenyewe lengo hilo huitwa Upimaji miliki (Cadastral Survey)

#### **Upimaji miliki mijini**

**1.**Maombi ya miliki yatawasilishwa kwa Afisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya, Jiji, Manispaa au Mji husika.

**2.**Afisa Ardhi atakagua eneo kuthibitisha kuwa:

i)Ardhi husika ina mchoro wa mpan-gomiji ulioidhinishwa.



Plani ya viwanja

ii).Ardhi husika ni huru, haina migogoro ya mipaka, miliki au hati iliyowekwa rehani.

iii)Ardhi husika haina upimaji uliotangulia na kama upo haikusudiwi kuu-tumia kumilikisha ardhi hiyo.

**3.**Afisa Ardhi atafanya mawasiliano na Mpima Ardhi wa Halmashauri husika kwa kujaza fomu SF 37 (Request for Survey) ikiambatanishwa na mchoro wa mipangomiji uliodhinishwa.

**4.**Mpima Ardhi wa Halmashauri attoa maelekezo ya Upimaji (Survey Instructions) kwa Mpimaji.

**5.**Baada ya upimaji kukamilika, nyaraka zote za upimaji huwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani kukaguliwa, kuthibitishwa na kusajiliwa kama kumbukumbu rasmi ya mipaka ya Ardhi husika.

**6.**Upimaji mijini huzingatia michoro ya mipangomiji na sio mipaka ya asili jinsi majirani wanavyokaa. Hapa ndipo umuhimu wa kuwa na ardhi huru unapoitokeza ili yeyote anayeathiriwa na utekelezaji wa mchoro wa mipango miji ashirikishwe kikamilifu iki-wa ni pamoja na kufidiwa kwa muju-bu wa sheria. Chini ya Sheria Sura Na. 324 (Sheria ya Upimaji ardhi) plani ya upimaji iliyoidhinishwa ndio uthibitisho rasmi wa mipaka ya ardhi iliyopimwa.

Hivyo, hatua ya kuomba upimaji, utekelezaji wake, ukaguzi, uthibitishwaji na usajili wa plani lazima viwe makini kuepusha matatizo kama vile miliki kutolewa juu ya nyigine .



### Upimaji Miliki Vijijini

Maombi ya upimaji ardhi yatawasilishwa kwa Afisa Ardhi wa Halmashauri. Afisa ardhi atachunguza na kuthibitisha ya-fuatayo:

- Ardhi iliyooombewa upimaji ni ya mhusika, ni huru na haina migogoro ya umiliki au mipaka.
- Iwapo Mhusika ni mwekezaji, kijiji kime-tenga ardhi hiyo ili **i Hawilishwe** kuwe-zesha kumilikishwa na Kamishna wa Ardhi.
- Kuna mihutasari ya vikao vya Halmashauri ya Kijiji vilivyopitisha maombi ya ardhi kwa mwekezaji.
- Vibali vya kumiliki ardhi kulingana na ukubwa wake vinapatikana katika naga-zi ya Kijiji, Wilaya, Mkoa au Wizara
- Afisa Ardhi atawasiliana na Mpimaji wa Halmashauri kwa kujaza fomu SF 37(Request For Survey) inayoambatana na mchoro wa ardhi inayoombewa

upimaji, nakala za muhtasari na vi bali vya kumilikisha.

• Upimaji unapokamilika, nyaraka zote huwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani kukaguliwa, kuthibishwa na hatimaye kusajiliwa kama kumbukumbu rasmi ya mi-paka ya ardhi iliyopimwa.

• Plani za hati (deed Plan ) huan-daliwa kutokana na plani za upimaji zilizothibitishwa. Plani hizi za hati huandaliwa na Ofisi ya Ardhi katika Halmashauri husika.

### Takwimu na Kumbukumbu za Upimaji Ardhi

- Idara ni mhazini wa takwimu na kumbukumbu za upimaji miliki nchini
- Kadi za vielelezo vya alama za msingi za upimaji
- Vipimo vya alama za msingi za upimaji
- Plani za upimaji miliki



Upimaji kwa kutumia kifaa cha GPS

### Takwimu na Kumbukumbu za Upimaji Ardhi

- Idara ni mhazini wa takwimu na kumbukumbu za upimaji miliki nchini
- Kadi za vielelezo vya alama za msingi za upimaji
- Vipimo vya alama za msingi za upimaji
- Plani za upimaji miliki